GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZUU NO. **254** Safar-R/Awwal **1447** AH Agosti– **2025** Zahoor **1404** HS BEI TSH 800/=

Kufuatia Jalsa Salana UK - 2025



UK. 09

Maadili ya Kiislamu katika Jamii ya Magharibi

Imetafsiriwa na
Maulana Sh. Mussa Bin Issa Sahib

Assalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuhu!

Ndugu zangu wapendwa, leo nataka kuzungumza nanyi kuhusu mada muhimu sana: Uhuishaji wa Maadili ya Kiislamu katika Jamii ya Magharibi.

Hakika, tunabahati kwamba Mwenyezi Mungu ametujalia kutupa fursa ya kuukubali Uislamu wa kweli kupitia Jamaat Ahmadiyya katika zama hizi. Uislamu ni dini ya ulimwengu mzima, mwongozo sio tu kwa Mashariki au Magharibi, bali kwa wanadamu wote. Mafundisho ya Qur'an Tukufu na mfano mwema wa Mtume[saw] unaonyesha kuwa alitumwa kwa ajili ya rehema kwa walimwengu wote. Sheria ya Kiislamu ilikamilishwa wakati wake, na leo, Mwenyezi Mungu ameikabidhi Jamaat Ahmadiyya jukumu la kuieneza. Hii inatimiza bishara ya Mtume[saw] aliyesema kuwa katika zama za mwisho, ambapo Uislamu utabakia jina tu, Mwenyezi Mungu atamwinua Hazrat Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa kwa ajili ya kuufufua.

Sisi sote tunaamini kwa yakini kuwa Uislamu utaenea duniani kote. Hata hivyo, tunapaswa pia kuwa na wasiwasi kwamba tusije tukaupotosha Uislamu wa kweli. Hazrat Muslih Maud[ra], alibainisha katika ziara yake ya mwaka 1924 Ulaya kuwa huenda Wazungu wakaukubali Uislamu, lakini wakauharibu na kuupotosha kabisa. Alisema huenda misikiti ikachukua nafasi ya makanisa, watu wakaheshimu

UK. 05

UONGO WA MASALAFI

Na: ALY KHAMIS JUMA WA PEMBA

UTANGULIZI

Mnamo mwezi wa tisa mwaka 2023 , nilipewa kijarida kiitwacho " UKWELI KUHUSU UKADIANI " ambacho ndani yake mna uwongo mwingi dhidi ya Ahmadiyya na kashfa nyingi dhidi ya muasisi wake , Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as].

Mwandishi wa kijarida hicho amejitambulisha kwa jina la Abu HALIMA Arafat wa Pongwe Tanga Tanzania .

Ingawaje kwenye kijarida hicho hamna jipya , bali ni yale yale tuliyo yazoea , na majibu yake yapo hadharani . lakini hata hivyo nimeonelea nitoe majibu yake kwani huenda Abu Halima anapenda na yeye jina lake liingie katika orodha ya "wapinzani waliojibiwa " ambao kwa hapa Tanzania ni pamoja na

Padre Dale - aliyetafsiri Kuran tukufu kwa Kiswahili.

Padre Anglas - aliyeandika kitabu WANA WA IBRAHIM

Sheikh Rizvi - aliyeandika kitabu Mtume[saw] ni Nabii wa mwisho .

Sheikh Abdalla SALEH

UK. 03



MAKHALIFA WA KI AHMADIYYA NA UHUSIANO WAO NA WANAJAMAATI

UK. 04

KUISHI MAISHA YA UNYENYEKEVU NA UMASKINI

UK. 08

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

IMANI JUU YA ALLAH


Maisha matakatifu ya Mtume[saw] ni kitabu kilicho wazi Kila ukurasa unaofungua na ukiusoma kwa makini unakufikisha kwenye ile shabaha mahususi ambayo ni kumwabudu Allah na kufika kwenye kilele cha kutangaza, "Maisha yangu, sala zangu na kifo changu ni kwa ajili ya Allah" Mtume[saw] ni mfano ulio bora kwetu sote. Imani yake kwa Allah ilikuwa ni muujiza mtupu. Allah Aliyemtambua, Kumtumikia na Kumpenda ni Yule Allah Aliyeelezwa katika Qur'an Tukufu; "Allah ni peke yake asiye na mshirika, uzuri wote unapatikana kwake. Allah ni nuru ya mbingu na ardhi. Ni chimbuko la wema wote. Yeye ndiye Aliyeumba Dunia na kuiendesha. Ni Yeye Aliyeleta kila kitu kutoka katika giza na kukipa nuru.

Hakuna chochote kilicho nje ya elimu yake, udhibiti au uumbaji. Hakuna kinachoweza kutokea bila Yeye. Na hakuna kinachoweza kuendelea bila ya msaada wake. Ana sifa ya kuumba, kuangamiza na sifa hizi hazijawahi kusimama. Sifa zote nzuri zimekusanyika kwake. Hana kasoro yoyote. Allah analipa kwa matendo yetu yote na kwake tutarejea. Yuko karibu na wakati huo huo Yuko mbali. Hakuzaa wala hakuzaliwa. Kwa sifa yake ya Rahmaan ametutayarishia kila kitu cha mahitaji yetu. Na hili limefanyika bila ya maombi yetu. Na kwa sifa ya Rahiim hulipa juhudi tunazozifanya. Huyo ndiye Allah ambaye Mtume[saw] aliyemfahamu na kumtumikia. Na Imani yake kwa Allah ndiyo ilikuwa maisha yake yote.

Kila tendo lake alilifanya kupata radhi ya Allah. Maadui wa Makka walifanya mpango wa kumuangamiza na zawadi zilitangazwa kwa atakayemleta mzima au mfu atapewa zawadi ya ngamia wekundu 100. Ulikuwa ni wakati mgumu na wenye hofu na wasiwasi mkubwa. Akiongozana na rafiki yake Seyidna Abubakar[ra] waliingia katika pango la 'thaur'. Mabingwa wa elimu ya kufuatilia nyayo walipiga mahesabu yao na walifika hadi pale pangoni.

Kwenye mlango wa kuingilia pangoni njiwa alitengeneza kiota chake na akataga mayai. Maadui walipofika hapo wakaanza malumbano kama hayuko hapa ndani basi amepaa mbinguni. Ndani mle pangoni Seyidna Abubakar[ra] alikuwa na wasiwasi na kutiririsha machozi kwa kuhofia usalama wa maisha ya Mtume[saw], lakini Mtume[saw] alimliwaza kwa kumwambia; "Usihofu wala usihuzunike, hakika Allah Yu pamoja Nasi". Imani yake ni kwamba, Allah katu hawezi kumuacha. Kuna kisa kingine alipokuwa anatoka katika moja ya vita, alijipunzisha chini ya mti mbali kidogo na Masahaba zake. Bedui mmoja aliona jambia lililokuwa limeegeshwa na akalichukua na mara Mtume[saw] akaamka na yule bedui akamuuliza Mtume[saw] nani anayeweza kukuokoa nami? Kwa sauti yenye Imani thabiti Mtume[saw] alijibu; "Allah". Yule bedui alianza kutetemeka na jambia likaanguka chini na Mtume[saw] akalichukua jambia na kumuuliza yule bedui; "Nani anayeweza kukuokoa" yule bedui akajibu "wewe". Hadithi zinaeleza kwamba Mtume[saw] alimsamehe bedui yule na kumuacha aende zake. Tizama Imani aliyokuwa nayo Mtume[saw] kwa Allah. Pameingia maradhi makubwa miongoni mwetu. Baada ya kuwa na Imani katika uwezo wa Allah, utasikia mtu anakwenda kwa mganga kwa sababu eti hajapata kazi na kuna mtu ambaye anadhani anamuwekea kauzibe. Huyu bila shaka hamuamini Allah ambaye Anaaminiwa na Mtume[saw]. Ukishampata Allah unahitaji nini tena? Tumtafute Allah ambaye baadhi ya sifa Zake tumezieleza hapo juu. Nje ya hapo ni hasara na kujitia utumwani kwa shetani.

Mbegu ya ushirikina haiwezi, katika ardhi ya Muaminio. Allah ambaye habari zake ametufundisha Mtume[saw] ndiye peke yake ambaye ni pepo kwetu. Tuitafute pepo hiyo kwa gharama yoyote iwayo kwa mustakbali mwema wa maisha yetu kiroho na kimwili pia. Na neno letu la mwisho ni; 'Sifa zote njema zinamhusu Allah, Mola wa ulimwengu mzima.




QUR'AN TUKUFU

هُوَ الَّذِیۡ بَعَثَ فِی الۡاُمِّیّٖنَ رَسُوۡلًا مِّنۡهُمۡ یَتۡلُوۡا عَلَیۡهِمۡ اٰیٰتِهٖ وَ یُزَکِّیۡهِمۡ وَ یُعَلِّمُهُمُ الۡکِتٰبَ وَ الۡحِکۡمَةَ ۚ وَ اِنۡ کَانُوۡا مِنۡ قَبۡلُ لَفِیۡ ضَلٰلٍ مُّبِیۡنٍ ۙ

وَّ اٰخَرِیۡنَ مِنۡهُمۡ لَمَّا یَلۡحَقُوۡا بِهِمۡ ؕ وَ هُوَ الۡعَزِیۡزُ الۡحَکِیۡمُ ۝

Yeye ndiye Aliyemwinua Mtume katika watu wasiojua kusoma, atokaye miongoni mwao, anawasomea Aya Zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hekima, na ingawa hapo kabla kwa hakika walikuwa katika upotevu dhahiri.

Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao; na Yeye ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.



NUKUU YA HADITHI

Kutoka kwa Abu Hurairah, kutoka kwa Mtume[saw] alisema: "Pua yake ifunge mavumbi, kisha pua yake ifunge mavumbi, kisha pua yake ifunge mavumbi!" Akaulizwa: "Nani huyo, ee Mjumbe wa Allaah?" Akasema: "Yule ambaye amewakuta wazazi wake wawili wanazeeka, mmoja wao au wote wawili, naye asiingie Peponi."



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

"Yeyote yule asiyewaheshimu wazazi wake na asiyewatii katika mambo yanayojulikana vizuri ambayo hayako kinyume na Quran, na asiyejali kuwahudumia, hayuko miongoni mwa jumuiya yangu." ***(Shafiq Nau', Ruhani Khazain, Vol. 19, ukurasa wa 19)***

Kuwahudumia wazazi ni tendo zito sana. Imeteremshwa katika Hadith Tukufu kwamba watu hao ni wenye bahati mbaya sana: mmoja ni yule aliyepata Ramadhani na Ramadhani ikapita lakini dhambi zake hazikusamehewa, na wa pili ni yule aliyewakuta wazazi wake na wazazi wake wakaaga dunia lakini dhambi zake hazikusamehewa. Mtoto anapokuwa chini ya kivuli cha wazazi wake, huzuni na masikitiko yake yote hubebwa na wazazi. Mtu anapojishughulisha mwenyewe na mambo ya kidunia, ndipo anatambua thamani ya wazazi. Mwenyezi Mungu amewaweka mama na baba mbele katika Quran Tukufu kwa sababu mama huvumilia maumivu makali kwa ajili ya mtoto. Ni nadra mtoto kupata ugonjwa wa kuambukiza. Kwa sababu wao ni watoto, wanakandamizwa, hawawezi kuacha mali...Mama na baba ni washirika katika shida za mtoto. Huu ni upendo wa asili, ambao hakuna upendo mwingine unaoweza kushindana nao. Mwenyezi Mungu ameashiria hili katika Quran Tukufu, akisema, 'Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu na wema na kuwapa jamaa' (Surah An-Nahl 91:16)." (Malfoozat, Juzuu ya 7, ukurasa wa 375, iliyochapishwa 1934)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

UONGO WA MASALAFI

Kutoka uk. 01

Farsi - aliyeandika kitabu Upotofu wa Tafsiri ya Makadiani Hao wote walijibiwa ipasavyo na ndipo wakafyata midomo yao . Sasa tunamsubiri Abu Halima tuone kama atathubutu kufumbua mdomo baada ya majibu haya . Wabillahi Taufiq
Mimi Aly Khamis Juma (Majani)

UWONGO WA MASALAFI

SURA YA KWANZA
UAHMADIYYA SI UKADIANI

Akianza uwongo wake Abu Halima ameandika : "Ukadiyani ni itikadi mpya iliyozuka mwanzoni mwa karne ya 14 Hijria, mwishoni mwa karne ya 19 Miladiya huko Qadiyyan , moja ya vijiji vilivyopo katika jimbo la Punjab nchini India " *(ukurasa wa 1 wa kijarida chake)*
Ni wazi kwamba Abu Halima anakusudia kuwataja Waahmadiyya kwani "Ukadiyani " unaishia hapo hapo katika kijiji alichokitaja , yaani Qadiyani.

Akifafanua zaidi ameandika: " Ama wafuasi wake wameitwa Makadiayani kwa ajili ya kunasibishwa na mji ambao alizaliwa kiongozi wa kundi hilo "
(ukurasa 1 wa kijarida chake)

Basi kwa mtazamo huu wa Abu Halima , masalafi jina lao ilitupasa tuwaite "Wanajdi " kwa sababu kiongozi wao Muhammad bin Abdul-Wahab anatokea Najdi . Kwanini basi wanajiita Masalafi?
Mbele kidogo ameandika:

" Na pia wanaitwa Ahamadiyya kwa ajili ya kunasibishwa na muasisi wa kundi hilo , ambaye ni Mirza Ghulam Ahmad " *(Uku.1 wa kijarida chake)*
Abu Halima haelewi au anaficha maksudi ni kwa nini tumeitwa Waahmadiyya . Sisi ni tofauti na wao Masalafi ambao wameitwa "Masalafi " kutokana na jina la kiongozi wao (muasisi) ambaye ni Muhammad bin Abdul Wahhab , wa Najdi .

Masalafi ni tawi moja miongoni mwa matawi ya" Mawahabi " Wengine wanajiita "Answar Sunna " wengine Hizbut – Tahrir n.k
Kwa faida ya wasomaji wetu , sisi tumeitwa Waahmadiyya kutokana na jina la pili la Mtume Muhammad[saw] " Ahmad " ambalo maana yake ni mwenye kusifu sana. Na Muhammad maana yake ni mwenye kusifiwa sana .

SURA YA PILI
UWONGO NDIYO KAZI YAO

Kijarida hiki cha Abu Halima kimejaa uwongo na matusi kwa mfano , ameandika:
"Mirza Ghulam Ahmad amezaliwa mwaka 1839 A. D" (UK 11) Sio kweli Mirza Ghulam Ahmad , masihi aliyeahidiwa a.s amezaliwa tarehe 13 Februari 1835 sawa na 14Shawwal 1250 Siku ya Ijumaa .
Uwongo mwengine wa hawa jamaa ni huu: "Na huwa wanaomba msaada kwa mataifa ya makafiri ili kupata nafasi nyeti Serikalini " *(ukurasa wa 4)*
Ni uwongo ambao hauna macho. Waahmadiyya hatuna tabia hiyo ya utegemezi.

Katika kila nchi tulipo , sisi ni raia kama raia wengine tunakula kwa jasho letu. Kisha Abu Halima ameandika : " Makadiyani wanaitakidi Tanasukhul Arwaah " (uk 10) Hatuna itikadi hiyo potofu . Hiyo ni itikadi ya Wahindu . Kuhusu itikadi hiyo Muasisi wa Ahmadiyya , Mirza Ghulam Ahmad (a s.) ameandika .
" Tunarudia maudhui yetu na tunasema kuwa jiha ya pili ya kubatilisha imani ya TANASUKH ni kuwa , hii ni kinyume cha utakaso wa kweli"
(hotuba ya Lahore uk. 34) .
Kisha Abu Halima ameandika :
"Wanaitakidi kwamba Allah anafunga anaswali , analala na anakosea "(uk 10). Huu wa Abu Halima ni uwongo uliotukuka , na kama ni mkweli tunamuomba alete ushahidi wa haya aliyoandika. Kuhusu habari hii , Mirza Ghulam Ahmad (a.s) anasema :-
"Kadhalika imo katika Kura-n tukufu kuwa Mungu ameepukana na kila aibu, yumbali na kila upungufu"
(Hotuba ya Lahore uk. 10)
Kisha Abuu Halima ameandika :-
"Wanaitakidi kwamba hakuna Qur-ani (ya kweli) isipokuwa ile aliyokuja nayo Masih Ghulam Mirza " (uk 10).

Huo nao ni uwongo mwengine wa hawa masalafi . Sisi hatujui Qur-ani nyingine zaidi ya ile iliyoshuka kwa Mtume[saw], na iwapo Abu Halima na Masalafi wenziwe wanaijua , tafadhali waiweke hadharani ili tupate kuhakikisha wanachokisema. Kuhusu Kur-an tukufu Mirza Ghulam Ahmad (a s) amesema :-
"Nasema kweli , tena nasema kwa kuapa kwa Allah kwamba , mimi na jumuiya yangu tuwaislamu , tunamwamini Mtume[saw] na Kur-an tukufu kama vile Muislamu wa kweli anavyostahili kuamini ". *(Hotuba ya Luviana , uk. 13)*

Uwongo mwengine wa Abu Halima ameandika: Wanaamini kwamba kitabu chao " ALKITAABUL MUBIIN ' kimeteremshwa kutoka mbinguni" (uk 11)
Sisi hatukijui hicho kitabu anachokisema , sijui yeye kakiona wapi . Atubainishie basi .Ajue tu Abu Halima huu tulio sio ulimwengu wa kudanganyana kiasi hicho .
Kwani vitabu vyetu vyote vipo hadharani kwenye mtandao , katika maktaba zetu n.k
Kisha ameandika "Wanaitakidi kwamba wao ni wafuasi wa dini mpya iliyo huru , na yenye ibada za kujitegemea " (uk 11)
Nadhani huyu Abu Halima anawadanganya vipofu na viziwi kwani Waahmadiyya , ambao kwa sasa tupo kwenye kila kona , tunaonekana tunavyofanya ibada , na pia tunasikika tunavyo hubiri , ambapo ni tofauti na haya aliyoandika Abu Halima , basi yeye haoni kwamba wasomaji wake watamuona mwehu ?

Sisi ni waislamu na ndio Waislamu wa kweli kwa nyakati hizi kwa maana tunakiongozi mwenye cheo cha KHALIFA anayetambulika mbinguni, kinyume na Waislamu wengine . Kinyume chake itikadi hiyo ni yao Masalafy:-
"Ingawa wao ni wafuasi thabiti wa itikadi ya Muhammad Abdul- Wahab lakini wanakana, wajibandika jina la Aswar – Sunna na hivi karibuni kujiita Masalafi huku wakidai kuwa wao ni Waislamu huru hawana imamu ."
(Upotovu wa Uwahhabi uk. 19)
Ameandika pia " Wanaitakidi kwamba Hija kubwa ni kutembelea mji wa Kadiyani na kuzuru kaburi la Mirza Al – *Qaadiyani "(uk 11) .*

Yaani ni uongo uliokithiri. Nadhani huyu jamaa ana shahada ya uwongo Lakini kusema uwongo si kazi , kazi ni kuuthibitisha huo uwongo . Na ndio maana uwongo wote alioandika hajathibitisha , na hawezi kuthibitisha kamwe .Basi auogope moto ambao kuni zake ni watu na mawe.

Kisha anasema. "wanahalalisha ulevi na madawa ya kulevya " Abu Halima ameishiwa hoja anajaribu kuitia dosari jumuiya hii lakini anakosa dosari za kweli anabaki kuhangaika . Sisi tuwaislamu, tunaiamini Kur-an tukufu yote , nayo Kur-an tukufu imekataza ulevi , iweje tena tuhalalishe kitu kilichoharamishwa na Kur-an tukufu?
Huo ni muhali kwetu . Kiongozi wetu , muasisi wa Ahmmadiyya ametufundisha hivi :-
"**Shabaha makusudi la ujaji wangu ni kuijadidisha Islamu na kuisaidia . Msidhani kwamba nimekuja na sheria mpya au nitoe maagizo mapya , au kitabu kipya kitashuka , hata kidogo. Sasa sheria yoyote mpya haiwezi kuja . Kur-an tukufu ni khaatamul Kutubi . Humo sasa hamna nafasi ya kupunguza au kuongeza hata nukta moja** ".
(Hutuba ya Luviana uk . 36)

Akiendelea na uwongo wake, Abu Halima ameandika kuhusu kifo cha Sayidna Ahmad[as] kwamba.
"Amefariki akiwa chooni anakidhi haja" (uk 20)
Akaongeza "Hivi ndivyo alivyokufa Mirza Ghulam katika hali mbaya ya kusikitisha " (uk 20) Almuradi ni kukashifu tu . Na hatushangai kwani hii ndio tabia ya wapinzani wa Manabii tangu zamani . Na Mtume[saw] alizushiwa kashfa nyingi tu . Kwa sababu ya mshikamano huu wa wapinzani wa Manabii .
Allah (sw) anauliza :
''JE WAMEUSIANA KUHUSU JAMBO HILI ? BALI HAWA NI WATU WAHALIFU "
(Surat Adhariati 51: 54)
Allah (sw) Anauliza , je hawa wapinzani wa Manabii wameusiana kwamba kila ajapo Nabii wa Allah wamdhalilishe ? Basi bila shaka Abu Halima na masheikhe wake atajibu "NDIYO"

SURA YA TATU
ALAMA ZA MNAFIKI

Zimethibiti alama za mnafiki kwa Abu Halima kama zilivyo ainishwa na Mtume[saw] aliyesema kwamba alama za mnafiki ni
1.Aongeapo husema uongo
2.Anapoaminiwa anafanya khiyana.
3.Anaposhindana anatumia matusi .
Katika sura ya pili ya makala hii tumeona jinsi Abu Halima alivyo hodari wa kusema uongo na sasa katika sura hii nitabainisha jinsi gani Abu Halima alivyo hodari wa matusi.

Kwa mwendelezo wa Makala hii piga simu au WhatsApp +255 658 971 662

MAKHALIFA WA KI AHMADIYYA NA UHUSIANO WAO NA WANAJAMAATI

Kutoka Uk wa 1..

Waheshimiwa wasikilizaji! Mada ya hotuba yangu ya leo, kama mlivyokwisha sikia, ni kuhusu uhusiano kati ya Khilafat Ahmadiyya na Jamaat. Leo hii tunapotazama hali ya dunia, kila mahali tunaona machafuko, vurugu, na kukosa amani. Sababu ya hali hii ni kwamba watu wamekataa kumkubali Imam wa Zama hizi, Masihi Aliyeahidiwa(as), na hivyo wamekosa neema adhimu ya Khilafa, kwa kushikamana na Kamba ya Mwenyezi Mungu (Hablullah) ambayo Jamaat Ahmadiyya imeishika imara, na kupitia hiyo ambayo inashuhudia fadhila nyingi zisizo na hesabu kutoka kwa Allah, ni neema ya Khilafa.

Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alitoa ushauri kuhusu umuhimu na ulazima wa kuwa na uhusiano wa kweli na Khalifa wa wakati. Kwa bahati mbaya, Waislamu wengi wa leo wamesahau mafundisho haya. Mtume (saw) alisema:"Kama utamuona Khalifa wa Allah duniani, basi jiunge naye. Hata kama mwili wako utakatwa vipande na mali yako kuchukuliwa."

Hadith hii inaonyesha wazi kwamba Khilafat ndiyo hazina kubwa na ya thamani zaidi duniani. Ni mali inayozidi uhai na utajiri. Kwa hivyo, pindi neema hii inapopewa Jamaat yoyote kutoka kwa Allah, basi ni lazima kushikamana nayo kwa hali zote — humo ndimo kuna uhakika wa maisha.

Uhusiano kati ya Khilafat Ahmadiyya na Jamaat umejaa upendo, mahaba na uaminifu — sawa na ule uliokuwepo katika Jamaat za mungu — na mfano kamili wa hilo ni ule wa Mtume Muhammad (saw) na Masahaba zake.

Mfano wa wazi ni Sahaba wa Mtume (saw), Zaid bin Dathinah (ra). Alipokuwa amekamatwa na makafiri kabla ya kuwawa, waliuliza:"Je, hungetamani kuwa salama nyumbani kwako na badala yake Muhammad (saw) awe yuko hapa mahali pako?"Kwa ghadhabu ya uaminifu, alijibu:"Siwezi kuvumilia hata kuona kwamba mimi nipo salama nyumbani huku mpendwa wangu Mtume (saw) akichomwa na mwiba katika mitaa ya Madina."Abu Sufyan aliposikia haya alisema:"Sijawahi kuona upendo kama huu!"

Waheshimiwa, hali kama hizi leo zinapatikana tu katika Jamaat Ahmadiyya.

Mfano wa hali hii ulionekana pia huko Canada, wakati Khalifa wa tano, Hazrat Mirza Masroor Ahmad (atba), alipozuru. Watu zaidi ya elfu tano — wanaume, wanawake, watoto, na wazee — walikusanyika saa moja kabla ya muda rasmi, wakisubiri kumuona Imam wao. Ghafla anga lilifunikwa na mawingu meusi, mvua kubwa ikaanza kunyesha, lakini kila mtu alibaki mahali pake, mvua ikiwanyeshea, wakimsubiri kwa hamu. Mavazi yao yalilowa, midomo yao ikawa ya buluu kwa baridi, miili yao ikitetemeka. Lakini kwa sababu ya mapenzi ya kweli kwa Khalifa, hawakujali mvua wala baridi. Hofu yao pekee ilikuwa:

"Je, mikono yangu iliyo na unyevunyevu huenda ikamsababishia maumivu Khalifa wangu mpendwa?"

Nchini Uganda, mama mmoja alikimbia pembeni mwa gari la Khalifa Mtukufu akiwa amembeba mtoto wake wa miaka miwili na nusu. Alikimbia kwa umbali mrefu, huku msongamano mkubwa ukiwa unasababisha asukumwe na kusukumwa, lakini hakujali. Hatimaye, mtoto alipomwona Khalifa Mtukufu, alitabasamu na kumpungia mkono wa salamu. Hapo ndipo mama yake alipohisi utulivu. Khalifa Mtukufu alisema:"Maadamu mama wa aina hii wataendelea kuzaliwa, ambao kwenye mapaja yao wanakuza watoto wanaoupenda Ukhalifa, Khilafat Ahmadiyya haitakuwa katika hatari yoyote."

Wakati wa Khalifa wa Nne, mwanamke mmoja wa kijijini kutoka Pakistan alitoa maombi ya visa ili aende London kushiriki Jalsa. Afisa wa visa alipomuuliza kwanini anataka kwenda, alijibu kwa unyenyekevu mkubwa:"Imamu wetu yuko huko, na kuna Jalsa, ndio maana nataka kwenda."

Alipoulizwa kama ana ndugu yeyote kule, alisema:"Ndiyo, mwanangu anaishi huko."Afisa aliposema, "Kwa nini husemi kwamba unaenda kumtembelea mwanao?" alijibu:"Mwanangu amekuwa huko kwa miaka 30, na sijawahi hata kuangalia upande huo. Lakini tangu Imam wangu alipohamia huko, moyo wangu haujapata utulivu na ninatamani mno kumwona Imam wangu."

Katika Jalsa ya Jubilee ya Khilafa, kutoka Burkina Faso, vijana 300 wa Khudamul-Ahmadiyya walifanya safari ndefu na ngumu kwa kutumia baiskeli chakavu hadi Ghana. Miongoni mwao walikuwemo watoto wawili wa miaka 13. Walipozuiwa kwenda, walilia na kusema:

"Lazima twende, tunataka kukutana na Khalifa wetu." Walipofika Ghana, walipoulizwa sababu ya kujitolea kwao kiasi hicho, Sadri wa Khuddam wa Burkina Faso alisema:

"Tulitaka kumuonesha Khalifa wetu kuwa hata hapa Burkina Faso, tuna vijana wanaompenda, wanaomwamini, na wako tayari kutoa kila sadaka kwa ajili yake."Huu ni upendo ambao Mwenyezi Mungu ameuweka ndani ya nyoyo zao.

Wasikilizaji! Kumbukeni, si sisi tu Wajamaati tunaowapenda viongozi wetu, bali upendo wa Khalifa wa wakati kwa Jamaat unazidi ule wetu mara nyingi zaidi.

Hazrat Khalifatul Masih III (rh) aliwahi kusema:"Jamaat na Imam wa Jamaat Ahmadiyya ni vitu viwili vinavyoitwa kwa jina tofauti lakini kimsingi ni kitu kimoja."

Hazrat Khalifatul Masih IV (rh), kabla ya kuhama kwenda London, siku moja aliwakusanya wanajamaat na akasema: "Sikuwaiteni hapa kwa sababu ya kuwatolea hotuba, bali nimewaita kwa sababu nataka kuwaona tu. Macho yangu hupata barudani na faraja kwa kuwaona, moyo wangu hupata utulivu. Nawapenda, nawathamini, na kwa jina la Allah, hakuna hata mama anayeweza kuwa na upendo wa aina hii kama nilionao kwenu."

Aliongeza:"Hamjatengwa nami — nyinyi ndio ulimwengu wangu. Kila sehemu ya maisha yangu imejaa kumbukumbu zenu. Enyi mnaoishi ndani ya pumzi zangu! Hamjawahi kutengana nami. Uhusiano huu ulioanzishwa na Allah utadumu daima."

Mara nyingi, huzuni ya kutengana na Wana-Ahmadi wa Pakistan ilimsumbua. Alisema:"Maumivu yaliyobadilika kuwa maneno yaliyojaa huzuni, labda yalilea katika kifua cha majonzi. Enyi wasafiri wa kumbukumbu, wenye ndoto za matumaini, mnaijaza mioyo lakini bado kuna ombwe lisilotimia. Tamaa ya kuwahisi karibu haikomi, shauku ya kuwaweka kando yangu imevuka mipaka."

Wakati wa Hazrat Khalifatul Masih I (ra), mke wa Choudhry Hakim Din alikuwa kwenye maumivu makali wakati wa kujifungua. Saa sita usiku, aligonga mlango wa Khalifa kuomba dua. Khalifa aliamka mara moja, akaingia ndani, akasoma dua juu ya tende na kumpa, akamwambia:

"Mpe mkeo tende hii, na unipatie habari pindi mtoto atakapozaliwa."

Choudhry Hakim Din anasimulia kuwa baada ya mkewe kula tende, muda mfupi baadaye alijifungua mtoto wa kike. Alipohudhuria sala ya alfajiri na kutoa taarifa, Khalifa alisema:"Hakim Din! Ulimpa mkeo tende, akajifungua, kisha mkalala kwa raha! Angalau ungenipa taarifa, ningelala kwa amani pia — nilikesha usiku mzima nikiomba dua kwa ajili ya mkeo."

Leo hii tunaye Imam mpendwa, Imam, ambaye huhisi maumivu yetu na hufurahia furaha yetu. Hazrat Musleh Maud (ra) alisema kuhusu hili:

"Kwa ajili yenu kuna mtu anayehisi maumivu yenu, anayewapenda, anayefanya huzuni yenu kuwa huzuni yake, anayefanya mateso yenu kuwa mateso yake, anayewaombea kwa Allah kwa unyenyekevu mkubwa."

Mtu mmoja kutoka Ujerumani alimwandikia Hazrat Khalifatul Masih V (atba) akimwambia kuwa mke wake hupoteza ujauzito wake kila anapofika mwezi wa tatu, na jambo hili limetokea mara tatu. Huzoor akasema:

"Kama ungenijulisha mapema, mtoto huyo asingeharibika. Sasa siku zijazo, Allah akikujalieni ujauzo, munijulishe mara moja, basi hakutakuwa na tatizo."

Baada ya muda, walipopata ujauzito na matatizo yalipoanza tena, walimpigia simu Khalifa Mtukufu kuomba dua. Huzoor akasema:"Vizuri mmenijulisha, InshAllah hakutakuwa na tatizo."

Kwa baraka za dua za Khalifa wa zama, walijifungua mtoto salama kabisa, na baadaye pia walibarikiwa na watoto wengine.

Mwaka 2006, wakati mwanajamaati mmoja mwaminifu kutoka Morocco alipokutana kwa mara ya pili na Huzoor (aba), Huzoor alimwambia:

"Mwaka 2005 nilipokwenda Hispania, nilipotembelea milima ya Gibraltar, niliwaona kwa mbali ndugu zangu wa Morocco. Nilisema 'Assalamu Alaikum' kutoka milimani."

Wasikilizaji, fikirieni tu — macho ya Khalifa yalipofikiria kwenye miji ya Morocco kutoka milima ya Gibraltar, aliwakumbuka waumini wake huko, na upendo wake kwao ulimfanya awaombee salama na baraka.

Katika mwaka 2008, Huzoor alipozuru Ghana, katika mojawapo ya siku za Jalsa, upepo mkali ulivuma jioni. Nguzo ya hema ilianguka usoni mwa kichwani cha binti wa mbashiri mmoja na akapata majeraha. Huzoor aliulizia mara kwa mara hali ya mtoto huyo. Siku iliyofuata walipoenda kukutana na Huzoor, mbashiri huyo alimleta binti yake moja kwa moja kutoka hospitali. Huzoor alimuulizia hali yake na akasema:"Nimekuwa nikiomba dua kwa ajili yako usiku kucha."

Hazrat Khalifatul Masih IV (rh) alipoonyesha upendo kwa Jamaat alisema: "Hamjui ni kiasi gani nahisi maumivu kila mmoja wenu anapoumia."

Waheshimiwa, huu ndio ukweli wa Khilafat ya kweli — moyo wa Khalifa unabeba mioyo ya Jamaat nzima. Maumivu ya Jamaat yanakuwa maumivu yake, na furaha ya Jamaat hukusanyika moyoni mwake.

Waheshimiwa! Uhusiano kati ya baba na binti hujaa hisia na mapenzi yasiyo na mipaka. Safiri moja, mtoto wa kike wa mwanajamati huko Rabwah aliposikia kuwa Huzoor amewapigia simu familia za mashahidi, alimwambia baba yake:

"Baba, laiti ungekuwa shahidi pia, basi simu ya Huzoor ingeingia kwetu pia."

Baba huyo alimwambia rafiki yake, na taarifa hii ilimfikia Huzoor (atba). Huzoor mwenyewe alimtafuta binti huyo na kumpigia simu. Akamwambia: "Huna haja ya kumtoa shahidi baba yako, mimi nitakutimizia haja yako hata bila ya hilo."

Nataka tujikumbushe tukio la miaka ya karibuni. Katika miaka michache iliyopita, zaidi ya 160 waumini

Endelea Uk wa 8..

Maadili ya Kiislamu katika Jamii ya Magharibi

Kutoka Uk 01..

zaidi tauhidi kuliko Utatu, wakamuheshimu Mtume[saw] zaidi ya Yesu, lakini bado wakaendelea na maovu ya Magharibi kama ngoma, maingiliano ya kiholela kati ya wanaume na wanawake, na unywaji wa pombe. Alisema Ulaya itabaki kama ilivyo, hata ikijiita ya Kiislamu badala ya Kikristo.

Ndugu zangu wasikilizaji, leo hii, katika jamii za Magharibi, tunapambana katika nyanja mbili kuu: ya nje na ya ndani.

Nyanja ya Nje: Jamii ya Magharibi inalenga kuingiza maovu yake kama uchi(kutokujisitiri), kutoamini Mungu(atheism), na kutokuwa na dini katika familia zetu ili Waislamu wasistahili tena kuitwa "umma bora".

Nyanja ya Ndani: Hii inahusiana na udhaifu wetu wenyewe, hasa katika suala la Pardah (hijabu). Kila mwanajumuia mwanaume na mwanamke anajua mafundisho ya Uislamu kuhusu Pardah. Hata hivyo, wakati mwingine kuna mapungufu – aidha kwa sababu ya waume kuzuia wake zao, shinikizo la jamii, au hisia za kujiona wako duni. Wengine hudhani kuwa Pardah itawafanya wake au binti zao wasikubalike katika jamii au kupunguza fursa zao za maendeleo. Hii ni ishara ya udhaifu wa kifikra.

Nawahakikishia, Pardah si kizuizi; wala si ishara ya udhaifu. Ni alama ya heshima, kujistahi, na utambuzi wa kiroho. Haizuii maendeleo wala haipunguzi uwezo. Bali huongeza msaada wa Mwenyezi Mungu. Angalieni mifano kama Dkt. Fahmooda Muneer aliyefanya kazi kwa muda mrefu katika Hospitali ya Fazal-e-Umar, Rabwah, huku akizingatia Pardah kikamilifu. Huzoor (ra) alisema kwamba yeyote anayetaka kujifunza namna ya kufanya kazi huku akizingatia Pardah ajifunze kwake. Vivyo hivyo, Dkt. Nusrat Jahan alikuwa mfano bora wa Pardah. Hata baada ya kupata elimu na kwenda London kila mwaka kuhuisha ujuzi wake wa kitaaluma katika kufanya ubobezi, aliendelea kushika Pardah. Hakuna aliyepinga, wala haikuathiri kazi yake au umahiri wake kitaaluma. Hata alifanya upasuaji mkubwa. Jambo la msingi ni hili: ikiwa nia ni kufuata mafundisho ya dini, njia daima zitapatikana.

Jambo jingine la wasiwasi ni kuiga bila kufikiri desturi za watu wa Magharibi, ambazo zimekuwa sehemu ya jamii hii. Kwa bahati mbaya, baadhi ya watoto wetu – wavulana na wasichana – wanaathiriwa na mambo haya. Miongoni mwa mambo haya ni kusherehekea siku za kuzaliwa, Siku ya Wapendanao (Valentine's Day), Krismasi, Siku ya Mwaka Mpya, na Pasaka. Hazrat Muslih Maud (ra) alieleza wasiwasi mkubwa kuhusu hili mwaka 1928. Alisisitiza umuhimu wa elimu ya dini, akisema kuwa ni elimu hii tu inayoweza kuwaokoa watoto wetu. Alishauri kwamba tusifuate tamaduni za Asia au Magharibi kwa upofu. Alisema tusishike Pardah kwa sababu ni ya Asia, wala tusiiache kwa sababu Ulaya haifanyi hivyo. Vile vile Khalifa Mtukufu wa 3(ra) mwaka 1975 alisema kuwa Pardah ni wajibu kwa wanawake na wanaume pia – akitaja amri ya Qur'an kwa wanaume kushusha macho yao.

Ndugu zangu wasikilizaji, kumbukeni kuwa dunia hii imejaa giza la Dajjal. Hila zake ni za ujanja, za kuvutia, na za kudanganya. Vyombo vya habari, tamaduni, kauli nzuri kuhusu "uhuru" – vyote hivi ni minyororo ya Dajjal. Lakini msihofu, mwishowe vyote vitashindwa mbele ya nuru ya Uislamu, InshaAllah. Hazrat Masih Ma'ood (as) aliwahi kusema akiwanasihi wafuasi wake kuwa, ni wale tu wanaoishi kwa mafundisho yake na kujitahidi kuyafuata ipasavyo hao ni sehemu ya wafuasi wake wa kweli. Alisema kujiandikisha kwa jina katika jumuia yake haitoshi; Mwenyezi Mungu amekusudia kuifanya jamaati hii kuwa maalum, na hakuna atakayebaki ndani yake kwa jina tu,kama hushikani jamaat kweli kweli.

Suluhisho kuu la mmomonyoko wa maadili katika jamii ya Magharibi ni Sala (Namaz). Qur'an inasema: "Kwa hakika Sala humzuia mtu na mambo machafu na maovu". Mtume Mtukufu (saw) alifundisha kuwa yeyote anayechukua udhu kisha akaelekea kwenye Sala, kila hatua huondoa dhambi na kuongeza thawabu. Aliyeswali nyuma ya Imamu kwa utulivu hufikia daraja ya juu peponi. Uhusiano wa kweli na Mwenyezi Mungu hupatikana kupitia Sala – hasa Sala ya jamaa. Bila Sala, hakuna uhusiano na Mwenyezi Mungu.

Hazrat Masih Ma'ood (as) alisema: "Sala ni haki ya Mungu; itimize kwa bidii. Hata kama familia yako yote itaangamia, usiache Sala. Sala inarekebisha imani, tabia, na mambo ya kidunia." Alisema Sala ni wajibu kwa kila Muislamu, na alipoulizwa na kundi lililotaka msamaha wa Sala kwa sababu ya biashara, alijibu: "Kama hakuna Sala, basi kuna nini? Hakuna imani bila Sala".

Hazrat Muslih Maud (ra) alionyesha wasiwasi kuhusu viongozi wa Jamaat kutozingatia Sala ya jamaa, akisema kuwa badala ya kuhimiza wengine, baadhi yao hawakuingia msikitini kwa wiki kadhaa. Alihimiza wanawake kuswali kwa jamaa endapo wanaume hawapo, na akina mama kuwapeleka watoto msikitini. Alisema kama hili litafanyika, jamaati itapata mwamko wa kiroho. Alisimulia tukio la utotoni ambapo Hazrat Masih Ma'ood (as) alimkemea vikali kwa kutohudhuria Sala ya jamaa,licha ya msikiti ulikuwa umejaa watu, tukio hili linaonyesha shauku ambayo sote tunapaswa kuwa nayo kwa ajili ya swala ya jamaa.

Ndugu zangu, mnapohamia nchi za Magharibi, ni muhimu msishawishike na hali nzuri ya kiuchumi bali mweke dini mbele ya kila kitu. Watu wengine huanza kwa kuhudhuria msikiti na shughuli za Jamaat, lakini polepole hujishughulisha na dunia na kuacha Sala. Hadithi ya Tha'labah bin Hatib Ansari, aliyesahau wajibu wake kwa Mungu baada ya kupata mali, iwe somo. Mtegemee Allah na kutanguliza dini mbele ya dunia ni msingi wa kiapo cha Jamaati Ahmadiyya. Nawahimiza kusoma masharti kumi ya Bai'at.

Mirza Masroor Ahmad,Amir Jamaat Ahmadiyya America aliwakumbusha wahamiaji kuwa sababu kuu ya wao kuhamia nchi za Magharibi ilikuwa kupata uhuru wa dini. Alionya dhidi ya kupoteza imani kwa sababu ya mapenzi ya dunia. Alisema kwamba kama huko nyuma walikuwa hawawezi kutamka Kalima kwa sababu ya hofu ya nguvu za kidunia, hapa wasije wakasahau Kalima kwa sababu ya mapenzi ya dunia. Alikemea wazazi wanaopuuzia malezi ya kiroho ya watoto wao.

Tauhidi ya kweli si kutamka tu "La Ilaha Illallah". Hazrat Masih Ma'ood (as) alifundisha kuwa Tauhidi ya kweli humgeuza mtu, huondoa chuki, husuda, na unafiki. Bila mabadiliko haya ya ndani, kutamka Kalima hakuna maana.

Hazrat Muslih Maud (ra) alionya vikali dhidi ya kuingiza maovu ya Magharibi na kuyaleta katika jamaati yetu. Aliwashauri vijana kuwa na sura ya muumini – kiimani na kimwonekano – na kuacha kuiga desturi za Magharibi. Alisema jukumu lao ni kubomoa ustaarabu wa Magharibi na kusimamisha maadili, utamaduni, na mila za Kiislamu.

Mifano mahususi ya athari mbaya za Magharibi ni pamoja na:

Wanaume kuvaa hereni, mikufu au kuchora michoro (tattoo).Wanaume kufuga nywele ndefu au kuonekana kama wanawake,Wasichana kuvaa kama wanaume au mavazi ya kufichua miili yao.

Mtume Mtukufu (saw) alisema: "Yeyote anayewaiga watu fulani ni mmoja wao."

Uislamu haupendi kuonyesha uzuri wa mwili kupita kiasi, kwani huleta maovu. Mambo mengine kama kufuga kucha ndefu, kusimama kichwa wazi, bila heshima (badala ya kufunika kichwa kama ilivyo desturi ya Kiislamu), pia ni mambo ya kuiga Magharibi ambayo Waislamu wanapaswa kuepuka.

Pia ni jambo la kusikitisha kwamba baadhi ya wazazi hukasirika watu wanapojaribu kurekebisha tabia zisizo za Kiislamu za watoto wao. Ni jukumu la kila Mwanajamaati kushiriki katika kurekebisha maadili ya watoto na vijana.

Hatimaye, hebu nitaje baadhi ya tamaduni za Kiislamu zinazopuuzwa kwa sababu ya athari za Magharibi na zinahitajika kufufuliwa:

Kusalimiana kwa "Assalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuhu" badala ya "hi" au "bye"

Kusema "Bismillah-hir Rahmannir Rahim" kabla ya kila jambo— kuanzia kufunga mlango, kula, hadi kutawadha. Kutumia mkono wa kulia kwa kila kitendo. Kuzingatia desturi kumi za kimaumbile (Fitrat) kama vile kupunguza masharubu, kufuga ndevu, kutumia miswaki, kusafisha pua kwa maji, kukata kucha, na kuondoa nywele za mwilini.

Wazazi wanapaswa kuwa makini sana na watoto wao kuhusu vipindi vya televisheni, maudhui ya mtandao, na filamu, kwani ukosefu wa udhibiti humwondoa mtoto kwenye njia ya dini.

Hebu tuwe na huzuni na maumivu kama aliyokuwa nayo Hazrat Masih Ma'ood (As) kuhusu hali ya Uislamu. Alikesha usiku kwa huzuni juu ya maafa ya Uislamu. Uhuishaji wa maadili ya Kiislamu si jukumu la maulamaa au viongozi wa Jamaat pekee, bali ni wajibu wa kila mzazi, kila kijana, kila mwalimu na kila mwanafunzi. Nyumba zetu lazima zibadilishwe kuwa vituo vya malezi ya Kiislamu. Na MTA ina nafasi kubwa sana katika hili. Lengo letu ni kuingiza upendo wa Mwenyezi Mungu, Qur'an, na Mtume Mtukufu (saw) mioyoni mwa watoto wetu.

Kumbukeni, jamii ya Magharibi, licha ya maendeleo yake katika sayansi, teknolojia, na utajiri, inakosa hali ya kiroho. Ninyi, wapendwa wangu, mmeitwa kuwa nuru katika giza, harufu nzuri inayosambaza upendo, na maji yanayozima kiu ya jamii hii.Lengo kuu la kuja kwa Hazrat Masih Ma'ood (as) lilikuwa ni kulea jumuiya ya waumini wa kweli— wanaomjua na kumwamini Mungu kwa dhati, wanaoishi Uislamu, wanaofuata mfano wa Mtume, wanaoishi kwa ucha-Mungu, na wanaosimamisha kiwango cha juu cha maadili. Ni kupitia jamuiya kama hii ndipo dunia itapata mwongozo, na mapenzi ya Mungu yatatimia.

Alisema kuwa ikiwa kusudi hili la msingi halitatimizwa, basi hata ushindi wa kielimu dhidi ya wapinzani kwa hoja na dalili hautakuwa na maana yoyote.

Mwisho, Namuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe sote kutimiza jukumu hili kubwa.

Wassalam.

Bustani ya Washairi

Haki sawa ndio nini

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Kila Kitu kiwesawa, maumbile tusawaze?
Majukumu yawesawa, Wana tuwanyonyesheze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze?
Kulima tufanye sawa, kupika nakozamuze
Sauti zipande sawa, siwepo naapunguze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Auviti viwesawa, vyeo tukigombeaze
Wasosifa kiusawa, mamlaka tuwajaze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Baba mama wawe sawa, sauti tuzipuuze
Nayemama awesawa, ubini tumuitize

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Au ndoa ziwesawa, mke namke tuoze
Wanaume naosawa, mume kwa mumetuoze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Mabingwa wahaki sawa, kinyume munieleze
Hukunaku kuwe sawa, mlingano idadize.

Mtunzi
M.O.kisagwa

Usikatae Mitala

Mjenzi ndiye mjuzi, kwakile alokiunda
Aloijenga kurunzi, mbali sana akakwenda
Akiba akamaizi, vifaa akaviunda
Usikatae mitala , mjenzi ndiye mjuzi

Hebu mwangalie kuku, jogoo alokomaa
Matembe wenyeshauku, dhamana humpatia
Waamsha mwanzo siku,namwewe kuwaambia
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Muumbaji anajua, ndiyo mana akasema
Rukisa wewe kuoa, wanawake walowema
Moja Hadi nne oa, kuzidisha sio wema
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Akili yako tumia, mitala ukizuia
Wale wanaobakia, utawa watatulia??
Kama hawatatulia, Nini Sasa chafwatia??
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Akili yako tumia, Nini kitachotokea
Usawa tukitumia, mitala kwa mke pia
Mimba mke kipatia, baba yupi atalea
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Kumbuka nakuambia, Kila mwana anababa
Jini wanazichangia, nusu mama nusu baba
Ugomvi utauzua, kugombania ubaba
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Hayo Kenda nakwambia, kumi hili lisikia
Siku zikishakujia, au mwana ukazaa
Waume tavumilia??au dhambi tawatia
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Mtunzi
Masihi omary stambuli kisagwa

MALI

Mali kitu azizi, ukiwa nayo moyo hutulia
Utakacho hufanyi ajizi, mara mkononi kimetulia
Hakuna wa kukushauri, umaizi,Mola riziki kakufungulia

Mali kitu azizi, hupewa walio barikiwa
Hapokonyeki hata kwa mizizi, alopewa kapewa
Wala hafanyi ubazazi, moyo wake umepowa

Mali imevunja nguu, na milima ikalala
Kisha ikamletea makuu, atakalo hukubaliwa
Kisha ikampandisha juu, serikali na raia

Mali inafungua njia, Makka waenda bila udhia
Upitapo waheshimiwa, jambo lako waitikiwa
Kisha waenda ukajisifia, nina akili kupindukia

Mali kitu azizi, katika Akhera na dunia
Mali itakuenzi, na sifa kukupatia
Wala usiwe m'bezi, usije ukaangamia

Mali itamu moyoni, utakacho wajinunulia
Mali itakupeleka Peponi, kwa njia rahisi kupindukia
Ama itakutupa Motoni, utachomwa na kuteketea

Mali kitu muhimu, kiumbe kuwa nazo
Zimejaa kwako darahimu, wala hupati majuto
Wageni wako tawakarimu, kwa tabasamu nzito

Mali itolee Zaka, ipate kutaharika
Yatakuepuka mashaka, mali yako itang'arika
Hutapata wahaka, mambo yote utafarijika

Mkono wa kupewa, hakika uko chini
Wanazuoni wametwambia, yapasa kuamini
Fukara huambiwa, yule naye wanini

Fukara hana shauri, matajiri hawamthamini
Japo anayo mazuri, hawamweki akilini
Dunia ina ghururi, uwe na yakini

Sifa zake tajiri, mfano wa ngamia
Imeandikwa tokea alfajiri, mfano anaosifiwa
Tundu ya sindano ikijiri, hawezi kupitia

Lakini yupo tajiri, sifa zake maridhia
Hafanyi ubakhili, hutoa kila pembe ya dunia
Huyo alivyo aali, sifaze sawa nabia

Mali tiba ya moyo, jingine haliwezikani
Mali fidia roho, wafarijika duniani
Huondoa joto la moyo, inakupa burudani

Mali si kila kitu, kaa ukifikiria
Wapata janga kuu, mali ikashindwa kufidia
Hayo siyo makuu, kwa Mola msifiwa

Yakupasa kula sasa

Tunajua unapenda, kunyonya umezoweya
Umuriwo umekwenda, hunabudi kuachiya
Shirina mbili sikenda, Miezi umetimiya
Yakupasa kula Sasa, na nyonyo kulisahau

Uji wa kukushikiya, ugali wakudonoa
Ubwabwa wakuviziya, vingine wakuonjea
Juisi wapendeleya, na vigumu tafunia
Yakupasa kula Sasa, na nyonyo kulisahau

Yakupasa kula Sasa, ugali nao msusa
Wali maharage Sasa, kuupenda yakupasa
Hakuna wakunyonyesha, hata sauti pazisha
Yakupasa kula Sasa, na nyonyo kulisahau

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

RAZAKI

Yeye ndo mgawa riziki, Huruzuku kwa mafungu
Pindi tupatapo dhiki, Na kughubikwa machungu
Tusisahau huyu rafiki, Mtibu yote machungu
Nakushukuru razaki, Mtufaa kila hali

Watupa tustahilicho, So kila kile tombacho
Tugawapo bila choyo, Wongeza kipunguacho
Twaafiki unenayo, Na turadhi upendacho
Nakushuru razaki, Mtufaa kila hali

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga
+255656557721
Email: shunda267@gmail.com

Mwenye nacho ongezwa

Tafuta uwe nacho, upate kujaziwa
Si tulie unacho, bila icho taporwa
Kikombe kuwa nacho, tatiliwa maziwa
Fumbua yako macho, fumbo kulitambuwa
Mwenye nacho ongezwa, duniani akhera.

Masihi omary stambuli Kisagwa (Masasi)

NJIA

Ni nzuri sana ajabu, siratwa ya katikati
Kaibariki Wahabu, kwayo Akatoa hati
Hivyo kwangu ni wajibu, rabeka Mola izati
Bora inashinda zote, chukua njia ya kati.

Na Mahmood Hamsin Mubiru –Wamamba Kiwalani - Dar es salaam.

Nguvu ya Ukweli

Vijana watatu wa chuo kikuu hawakufanya mtihani kwa sababu hawakusoma na hawakujiandaa.

Wakaja na mpango, wajichafue na oil chafu kisha waende kumwona mwalimu wao wa chuo.

“Mwalimu tunaomba samahani hatukuja kwenye mtihani. Tulikuwa tumehudhuria harusi na wakati tunarudi gari letu lilipata tatizo na hivyo tukachafuka sana kama unavyo tuona”. Mwalimu wa chuo aliwaelewa na akawapa siku tatu wajiandae.

Baada ya siku tatu, walienda kwa Mwalimu wao wa chuo wakiwa wamejiandaa vizuri kwaajili ya mtihani maana walikuwa wamesoma.

Mwalimu wa chuo aliwaweka kwenye madarasa matatu tofauti na kuwapa maswali manne tu kwenye karatasi ya mtihani;

1. Nani alikuwa anaoa au kuolewa? (Alama 25)
2. Sherehe zilifanyika wapi? (Alama 25)
3. Ni wapi hasa gari lilipopata tatizo? (Alama 25)
4. Gari ilipata aina gani ya tatizo?(Alama 25).

Majibu ya kusahihishia: Majibu yenu lazima yafanane.

Hivi tunavyoongea bado wapo kwenye mtihani.

Somo: Ifahamu kweli nayo kweli itakuweka huru.

TAFUTA WANYAMA SITA KATIKA MCHORO

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____
6. _____



JINSI YA KUPIKA MAANDAZI

MAHITAJI YA MAANDAZI

1. Unga - 5 Vikombe.
2. Tui la Nazi zito vugu vugu - 1 ¼ kikombe.
3. Sukari - 3/4 kikombe cha chai.
4. Samli iliyoyayushwa au mafuta - 3 vijiko vya Supu.
5.Hamirah - 2 Vijiko vya Supu.
6. Hiliki - 1/2 Kijiko cha chai.
7. Mafuta ya kukaangia.



NAMNA YA KUTAYARISHA NA KUPIKA.

1. Ndani ya kibakuli kidogo, mimina hamira na na vijiko viwili vya kulia vya tui. Weka kando mpaka hamira ianze kufura, kama dakika 5-10.

2. Pasha samli moto:
3. Ndani ya bakuli kubwa au sinia, changanya unga, sukari, iliki na samli ikiwa bado moto moto.
4. Mimina hamira ndani ya mchanganyiko wa unga.
5. Changanya na ukande huku ukitumia lile tui la nazi. Tui likipungua unaweza ukaongeza maziwa.
6. Kanda unga mpaka uwe laini.
7. Kata madonge *12 au 15 uyaweke kwenye baraza iliyonyunyiziwa unga na uyafunike ili yapate kufura na yasikauke.

Ukipenda maandazi manene fanya madonge 12.

MAKHALIFA WA KI AHMADIYYA NA UHUSIANO WAO NA WANAJAMAATI

Kutoka 04

waaminifu walitoa maisha yao kwa ajili ya Khilafat Ahmadiyya — huko Lahore, miji mingine ya Pakistan, Indonesia, na Burkina Faso.

Mashahidi hawa walifufua historia ya Masahaba wa Mtume Muhammad (saw) kwa kutoa damu yao katika njia ya Allah. Walitoa ujumbe kwa wafuasi wa nidhamu hii ya ukhalifa duniani kote:

“Ahadi tuliyoitoa ya kuilinda Khilafat tutaitimiza. Sisi tunaondoka duniani,Sikilizeni nishani hii (Ukhalifa) ya Hazrat Masih Maud (as) sasa wajibu huu uko mikononi mwenu ni faradhi kulinda amana hii!”

Katika siku hizo za kujitolea, uhusiano kati ya Jamaat na Khilafa uliinuka kwa hadhi mpya.Kwa upande mmoja, Huzoor alipiga simu binafsi kwa familia za mashahidi, akawafariji. Kwa upande mwingine, sio familia hizo pekee bali Jamaat dunia nzima ilifanya upya ahadi ya utii na uaminifu kwa Khalifa kwa nguvu mpya, ujasiri mpya, na mapenzi mapya:”Ewe Khalifatul Masih! Tupo pamoja nawe! Kwa ajili yako na Khilafat Ahmadiyya tupo tayari kutoa tone letu la mwisho la damu, InshAllah!”

Bahari hii ya mapenzi ya kweli ilikuwa pia ujumbe wa wazi kwa maadui:

“Kila mnapojaribu kutuvunja, tutarudi tukiwa na nguvu zaidi!”

“Mnapoota kututenganisha na wapendwa wetu, mkitaka kutugawa na kutuvunja, mtakutana nasi tukisimama nyuma ya Imam wetu kama ukuta wa chuma, tulioungana na thabiti — InshAllah!”

Nataka kuwaambia wale watu wanaojaribu kwa njia ya mtandao kuwavuruga kiakili Wanajamaati wasio na hatia, wakidhani kuwa kwa kupambana na Khalifa wa zama wanaweza kuidhoofisha Jamaat, basi wakumbuke — na wakumbuke vyema — kwamba vitendo vyao hivi vitakuwa mbolea ya kukuza uaminifu wa kweli na mapenzi ya Jamaat kwa Khilafat. Jamaat itaendelea kusonga mbele kwa mafanikio makubwa zaidi chini ya miguu ya Khilafat.

Ni wao wanaopaswa kujiuliza, wale waliowahi kupambana dhidi ya Khalifat waliitwa kwa jina gani? Bila shaka, asiyeitii Khilafat huitwa shetani. Na kama walivyoshindwa na kudhalilika huko nyuma, ndivyo ilivyo leo na ndivyo itakavyobaki InshaAllah. Watu wa aina hii wanapaswa kukumbuka kwamba Qur’an Tukufu imelitumia neno “Fasiqun” kwa watu kama hawa katika Ayat Istikhlaf. Huzoor amesema:”Wanapaswa kutafakari wale ambao hawathamini neema ya Khilafa.””Si Khilafa itakayoanguka kutoka daraja lake, bali ni wale wasioutambua utukufu wa Khilafa ndio watakaohesabiwa miongoni mwa waasi (fasiqun).””Wataangamia wale wasioelewa nafasi ya Khalifat au Khalafa.”

“Kumbukeni kwamba hata wanafiki waliopita walikuwa werevu kuliko ninyi, lakini wote walikufa kwa aibu. Mipango yao yote ilishindwa, na sasa majina yao yanatajwa tu kama funzo. Ikiwa mtachukua njia hiyo hiyo, basi msitarajie mwisho tofauti na huo.”Kila mmoja hupata hifadhi chini ya kivuli hiki — angalia jinsi vazi la Khilafat lilivyo pana!”

Uaminifu ndio tabia ya wafuasi wa Khilafati, na kiapo cha Khilafat kinategemea utii.

Hazrat Khalifatul Masih V (atba) anasema:”Ni kiongozi gani wa dunia anayewaombea wagonjwa? Ni kiongozi gani anayehangaika kwa ajili ya mabinti wa taifa lake? Ni kiongozi gani anayetamani kuwaona wakiolewa kwa furaha na kuwaombea dua? Ni kiongozi gani anayejali elimu ya watoto?”

Huzoor anasema:”Hakuna nchi duniani ambayo akili yangu haifiki kila usiku kabla sijalala. Nawaombea dua wakiwa ndani ya fikra zangu usiku na mchana.”

Katika hitimisho la hotuba yangu, naweza kusema kwa yakini kamili — hili ni jambo la milele — kwamba hata kipande cha udongo kinapoguswa na jiwe la thamani la Khilafat, hubadilika kuwa almasi. Wafu hufufuka, na roho zinazotengwa na Khilafat hubaki katika udhalili daima.

Kumbukeni daima, Khilafa ni mwangaza katika giza. Na dua za Khalifa wa wakati ndizo hutuliza mioyo. Uongozi wake hubadilisha hali ngumu kuwa mafanikio. Lakini jambo moja kila mmoja lazima akumbuke daima: Dua za Khalifa huonekana kwa kweli tu kwa yule aliye mpenzi wa kweli na mtiifu wa kweli kwake.

Waheshimiwa! Hebu twende sote kwa pamoja tukimthibitishia upendo wetu Imam wetu mpenzi. Tuseme kwa sauti moja:

“Ewe Kiongozi wetu mpenzi! Kila utakapotuita kwenye njia ya wema, tuko tayari kujitolea maisha yetu kwa ishara zako. Maisha yetu na mauti yetu zitakuwa miguuni pa Khilafa.”Hazrat Khalifatul Masih V (atba) anasema:

“Mkitaka ibada zenu, wema wenu na kazi zenu zote zifikie mwisho wenye baraka, basi fanyeni mapenzi na heshima kwa Khilafat kuwa sehemu ya imani yenu.”

“Na jambo hili lijengewe ndani ya mishipa ya damu ya vizazi vyenu, kwamba maendeleo yenu yote sasa yanahusiana moja kwa moja na Khilafa.”

“Mfuateni kwa bidii, fanyeni ishara zake kuwa amri zenu, na mtashuhudia mafanikio na ushindi vikiwasujudia InshaAllah.”

Allahumma Amin

MATUKIO KATIKA PICHA











SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Kutoka Uk.12

ushuke chini baada ya kushuka katika treni na ni kawaida kupanda lifti ilikupita daraja la juu kuvuka barabara au kwenda kwenye stesheni ya reli. Wale wabashiri wawili tuliongozana nao waliokuwa watu wachangamfu na wanyenyekevu mno, nilikuwa naona katika nyuso athari ya mazingira yao kwani wahindi wanaukali wa hali ya juu lakini pia ni wapole mno, wabashiri hao mavazi yao na jinsi tulivyoongazana nao kwa mazingira ya kwetu unaweza sema chambilecho cha vijana wa kileo kuwa mwandishi na weziwe kuwa walikuwa washikaji sana.

Tulipofika katika kituo cha kwenda kubadili fedha tuliamua wenzetu wawili waende na mwenyeji mmoja na sisi wawili tulibakia na mwenyeji mmoja na tuliamua kusubiri ili kufanya jambo kuwa rahisi. Hivyo Mimi na Shekh Husein Ng'amilo tulibaki pamoja na mwenyeji mmoja, na Sheikh Ayyaz Ahmad na Sheikh Tahir Marunda waliongozana na mwenyeji wetu kwenda kubadili fedha. Walipoenda walipata fursa ya kutembelea kaburi **Nizamuddin Auliya** ambaye alikuwa ni walii mkubwa wa Mungu na sufi mkubwa na pamoja naye yapo makaburi mengine, sehemu hii Saydna Ahmad (as) alitembelea na kufanya maombi katika zama za uhai wake. Kwa bahati nzuri tulipokuwa Delhi katika markaz ya jumuiya alikuja mzee mmoja na katika maongezi naye alijitambulisha kuwa yeye ni mlinzi wa Huzoor (aba) anapotembelea nchini India na aliambatana naye mwaka 2005, Huzoor (aba) alienda kutembelea katika makaburi haya na kufanya maombi na cha ajabu zaidi ni kwamba Huzoor (aba) aliwapa hela wale wote wanaokaa katika maeneo haya na kuomba omba na kuimba kasida za namna mbali mbali. Muujiza zaidi ni kwamba Huzoor (aba) alipofika tu watu wote walimpisha na kuanza kumshangaa yeye na wote kukaa kimya na sehemu hii asili yake ni fujo na msukumano, Huzoor (aba) aliulizwa kuhusu kuwapa hela, akasema ni kwa sababu watu hawa wapo hapa wakinadi na kuimba jina la Allah na Mtume wake (sa), na kwa bahati nzuri makala iitwayo **Apney desi main** imeonyesha mandhari hii yote kwa uwazi sana na kueleza kuwa Huzoor (aba) ametembelea eneo hili baada ya miaka mia moja baada ya Saydna Ahmad (as) kutembelea na aliwapa hela ombaomba wa pale kama alivyofanya Huzoor (aba) na hakuna yeyote aliyejua hilo kabla ya hapo na wala ziara hii haikuwa imeandaliwa katika ratiba.

Wenzetu waliporudi walitutambia mpaka nikajihisi mdogo kwa huzuni, Yule mbashiri tuliyebaki naye tulipoanza kuongea naye ndio tukajua ni Naibu Nazir Islah o Irshad senior Mubalighiin wa India, tunaweza sema mashekhe wote waliotumikia muda mrefu nchini India wapo chini yake, jambo la kustaajabu alivyokuwa anahangaika kutupiga picha katika safari hii na tulivyokuwa anatuongelesha kawaida ilihali ofisi yake huko Qadian huwezi kuifikia mpaka kuwe na sababu maalum na uwe Sheikh wa kaliba anayoshughulikia, na wakati wa Jalsa Salana yeye alikuwa anasimamia idara ya Langar Khana namba tatu ambayo inapika chakula cha wageni wa nje yaani wa kimataifa na pia ndipo palipo na ule mtambo wa kutengeneza chapati. Ubaya ni kwamba unapotambua cheo cha mtu ndio heshima huja juu yake na kuanza kumhudumia sawa na daraja lake, japo hatukufanya chochote cha kumuonyesha sisi ni maulamaa lakini huduma aliyotupa ilitufanya tujisikie ametoka nje ya mipaka yake na kutuhudumia kupita kawaida bila kujijali wala kujisikia, namuomba Mwenyezi Mungu anisamehe sana, somo hili nimelielewa. Daima Allah amjaalie moyo wenye unyenyekevu na huruma.

Basi safari ya sokoni ikaanza tukaelekea Jama Masjid ambapo kuna soko siku ya jumapili kama gulio lakini soko linakuwepo siku zote, soko ambalo liko barabarani, watu wamepanga vitu kando kando na katikati na kutengeneza njia mbili kwa wanunuzi. Wenyeji wetu kila tulipotaka kuuliza bei na kununua bidhaa walianza kuongea lugha ya kihindi na muuzaji kilichofuata baada ya hapo ni kwamba tuondoke jamaa anauza vitu ghali, upande wetu muuzaji alipokuwa akisema bei tunaangalia ni shilingi ngapi na tunalinganisha bei ya kitu hicho nchini kwetu tunaona bei ni rahisi mara tatu zaidi, lakini wenyeji wetu wanatuambia achaneni naye anauza vitu ghali mno na tunaendelea mbele, tumemaliza soko lote bila kununua chochote kwa mfumo huo.

Kwa ujumla wahindi ni wafanya biashara wazuri mno, siku ile tulichokuwa tunakiona ni kwamba mtu alikuwa akiuliza bei sana na kumsumbua muuzaji, basi muuzaji alikuwa akimuambia basi nenda, kinachosemwa sawa na wataalamu wa uuzaji ni namna nzuri ya kuuza ukiona mteja sio mnunuaji basi ni bora ukamuambia aende, lakini pia baada ya kukaa kwa muda fulani India na Qadian nimeona kwamba muuzaji mhindi ana uwezo wa kumsikiliza mteja mno na kumuonyesha bidhaa za duka zima bila kuchoka. Mfano anaweza kukutafutia kiatu mpaka upate unachokipenda, na akishapata unachokipenda anafunga vingine vyote na kuongea na wewe mpaka ununue kile ulichokipenda kwa namna yeyote iwayo utanunua tu hata kwa kukopa. Nakumbuka siku moja shemeji yangu Sheikh Tahir Marunda sahib alienda sokoni alikuwa anataka kununua blenda (mashine ya kusaga) ya mkononi ya kusagia matunda ila alirudi na chupa ndogo ya kunywea maji ambayo inahifadhi maji ya moto au baridi kwa bei ya 600 RS, akajisemea kwamba 'nimeenda kununua blenda ila nimerudi na hii chupa kwa sababu ya nguvu ya uuzaji wa wahindi'. Vivyo hivyo binafsi nimenunua vitu kadhaa ambavyo sikuvihitaji ila kwa sababu ya nguvu ya ushawishi. Kuna mifumo ya uuzaji wanayoizingatia moja ni ukiona mteja ameshavutiwa na kitu kimoja basi inatakiwa kuongea naye mpaka mfikie muafaka na anunue ile bidhaa iwe ni kwa kuamua au kwa ushawishi.

Msanii Rick Ross wa Marekani ambaye aliulizwa katika kipindi kimoja kuhusu siri ya utajiri wake akasema kwamba siri ya utajiri wake ni njia yake ya uuzaji. Kwamba yeye ana kiwango chake cha bei inayojulikana kama unamuhitaji sehemu yoyote lakini mtu anapokuja na fedha pungufu huwa hayupo tayari kumuacha aondoke na hiyo hela, atampa huduma ya kiwango cha hela yake au kumshawishi kwamba hela nyingine atamletea baadaye. Yeye hufanya matamasha makubwa lakini hajiachi kuwa huru siku za kawaida ambapo hana tamasha kubwa anapita kutumbuiza kwenye maharusi na vikao binafsi vya familia na sehemu za starehe ambapo anakusanya hizo fedha ndogo ndogo mpaka zitakapofika siku za matamasha makubwa. Binafsi naona wengi wetu tunajifunga kwenye viwango na thamani na sio kutoa huduma tukisimamia msimamo wa kulinda brand.

Kuna namna ya uuzaji alielezea vizuri mno Vusi Thembekwayo mjasiriamali na muandishi kutoka Afrika kusini katika madarasa yake ya mtandaoni alipomuuliza mfanya biashara wa urembo kuwa anampamba mtu kwa shilingi ngapi, alipomjibu kima chake, akamuuliza kuwa tena je mtu akija na kiwango pungufu itakuwaje akasema 'nitamuelekeza sehemu ambayo anaweza kupata huduma sawa na kiwango chake cha fedha', akaitika sawa sawa, akamueleza je itakuwaje ukianza kumuuliza kuwa unajiremba kwa ajili ya nini labda atakuambia anaenda kwenye sendoff ya rafiki yake, ukamuambia unaenda kufanya urembo wa bei rahisi je ikitokea aliyekuwa mpenzi wako yupo kwenye hiyo shughuli si atakuona mtu rahisi kabisa na usiyevutia kwa sababu umefubaa, yaani namna hii unamhamisha mtu kutoka kwenye kununua mpaka kwenye thamani yake na atachokuwa anawaza ni Yule mpuuzi aliyekuwa mpenzi wake kumkomesha na kumuonyesha amepanda thamani. Namna hii aliyoelezea ni njia bora ya kuuza bidhaa kwani mtu hununua thamani na sio bidhaa.

Kuna Mzee moja wakati wa Jalsa salana Qadian inaendelea nilienda kununua kofia ya kujikinga na baridi nilipofika alikuwa anamuuzia jamaa Fulani bidhaa hiyo hiyo, nilipomwambia kuwa nataka kofia ya namna hiyo hiyo aliniambia kwa ishara kuwa nitulie kwanza amalize biashara na jamaa wa kwanza, alipomalizana na jamaa wa kwanza ndipo akanitolea. Tukaanza kuzungumza bei ikiwa wale walionunua bidhaa kama ninayoitaka washaondoka. Nayo hii ni namna nzuri mno ya kuuza kwa sababu kuna wateja wengine hasa katika kununua bidhaa wakiona rangi au bidhaa nyingine maoni yao huanza kuyumba.

Kuna jamaa mmoja alikuwa anazungumzia siri ya kuuza katika mahojiano Fulani, akasema kwamba katika vitu viwili mara nyingi mtu anaweza kuchagua kimoja na kukinunua na katika vitu vitatu mara nyingi kuna uwezekano wa kutokununua chochote. Akasema kwamba kulikuwa na mzee Fulani alikuwa anauza viatu na alipata mafanikio mno, na siri yake ya kuuza ilikuwa hii kwamba alikuwa anamsikiliza kwanza mteja kitu anachotaka na anamletea pea mbili na kumuambia achague moja kati ya hizo kisha wanaongea naye biashara.Hizo ndizo namna ya kuuza.

Ukurasa wa 11

SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Kutoka uk. 11

Kuna muandishi aliandika kitabu akielezea kuwa kuuza ni utu, kwa sababu watu hununua kwa watu wanaowaamini na kuwapenda pia, katika zama zetu hizi maadili ndio yanayowaangusha watu katika biashara, hakuna mtu ambaye atataka kufanya biashara na mtu mwenye ndimi mbili au mwenye muonekano wa ubazazi. Wengi wanaeleza kwamba kama kijana ukitaka kufanya biashara kufanya mazoezi ni muhimu, ingia jimu tafuta muonekeano mzuri ili kila nguo iwe inakukaa vizuri na hata ukitokea kwa mbali waone mtu ambaye anajiweza na kujielewa. Saikolojia ya kuuza ni utu imefikia hapa kwamba watu wa dunia imemuweka mbele mwanamke katika kila biashara, yaani ukitaka kufanikiwa katika biashara basi mwanamke ndio aitangaze biashara hiyo au awe mbele katika biashara hiyo, mwanaume moja kwa moja anavutiwa na mwanamke na anashindwa kuelewa kuwa anavutiwa na biashara anayofanya au amevutiwa na muuzaji. Upande wa wanawake wenzie ni rahisi kwani kampeni za mwanamke kumsaidia mwanamke mwenzie ni jambo la kila siku, hivyo basi biashara inaonekana kuwa mwanamke ndio mshawishi, muuzaji na msimamizi, lakini la muhimu na ukweli ni kwamba kama ukitaka kufanikiwa katika biashara basi uaminifu, ukweli na juhudi ndio kila kitu.

Wahindi ni watu waaminifu mno, tulienda kwenye mgahawa Fulani mzuri wa wahindu ambapo alitukaribisha na akatuletea menyu (orodha ya chakula). Kiukweli msomaji wa menyu alikuwa haelewi vyakula vile vilivyoainishwa, nami nilipoangalia sijaona vyakula ninavyovijua lakini majina yalikuwa yanaendana. Alipokuja Yule mhindu na kutuona ni waislamu alikuwa ameleta maji na glasi tayari, lakini alitutanabaisha kuwa katika mgahawa wake hawauzi vitu halali na kama tunataka vitu halali basi tuende mgahawa Fulani na Fulani. Nikajisemea moyoni, 'sisi ni wageni angeamua kukaa kimya na kupata hela yake kingeharibika nini'?. Lakini ni kinyume na roho ya kibiashara kuuza bidhaa yenye athari mbaya kwa mteja, na wahindu hasa wapunjab wanaheshimu sana wageni na ni wakaribishaji wazuri wa wageni.

Nilichokiona ni kwamba maduka na migahawa mingi niliyoingia ilikuwepo tangu enzi za mababu na mababu, na utaona picha ya muanzilishi wa mgahawa huo ukutani na wote waliorithiana, wanachokifanya ni kwamba sio kumrithisha tu mtoto utaalamu na biashara, bali baba anakuwa na biashara moja ambayo anaiweza kweli kweli anaendelea nayo na kuipanua, mfano labda anaanza na kuuza chai na vitu vitamu akiwa na meza moja, hivyo basi kwa kuwarithisha vijana wake na muda kupita duka linatanuka na mpaka wamefikia kuwa na vifaa vya kisasa vya kutengeneza hizo bidhaa zao na kutoa huduma. Utakuta wengine duka zima wanatengeneza maboksi peke yake ya kufungia bidhaa, nilienda kwenye duka Fulani ambapo ndio sehemu pekee unaweza kupata vifaa vya kushonea nguo kuanzia mashine mpaka sindano na uzi. Katika masomo ya kibiashara kinachosemwa ni kwamba utafute kitu ambacho unakiweza kukifanya vizuri ukikuze na kukifanya chanzo cha kipato chako kwa kuchagua unachokiweza zaidi utakipenda na utakifanya kwa ustadi na utastarehe katika kukifanya. Wenzetu wahindi utakuta baba ameanza kazi ya udobi kwa kufua kwa mkono lakini aliendeleza na kuirithisha mpaka utakuta wanafua kwa vifaa vya kisasa na utakuta walianza na fremu moja lakini sasa wanamiliki jengo zima. Sisi waafrika hatuna tabia ya kurithishana kitu chochote na hata tukirithi basi tunagawana na kila mtu kuanza upya.

Bila shaka katika soko lile la Jama Masjid tulinunua baadhi ya bidhaa mbali mbali hasa za kujikinga na baridi, kwani wenyeji walishatumbia kuwa Qadian mvua imenyesha na nguo tunazozivaa Delhi hazitatufaa huko Qadian.

Lakini wote kiu yetu ilikuwa ni kuingia Jama Masjid na wenyeji wetu walikuwa hawajafika maeneo haya pia, tulipoingia ndani msikiti huu ulinipa taswira kwamba falme za kiislamu zilikuwa tajiri mno kipindi hicho, na usanifu majengo wake ulikuwa wa kiwango cha juu mno, uzuri na ukubwa wa jengo unasema wenyewe kuwa hii ni ngome ya ufalme imara na ni nadra sana kwa hali zetu za sasa kuweza kujenga jengo la namna hiyo japo tunazo nyenzo nyingi. Kwani Jama masjid ilijengwa kati ya 1644 – 1656 katika ufalme wa kimughal chini ya mfalme Shah Jahan.

Naona ni bora nieleze hili kwamba Mwenyezi Mungu huondoa elimu na utaalamu kwa kuhalikisha kaumu na vizazi Fulani. Kwa sababu kiu na ndoto ya kufanya vitu Fulani inakuwa katika mawazo na vifua vya watu, watu hao wanapofariki basi kila kitu kinakuwa kimeondoka. Mfano unaposoma maoni yote kuhusu ujenzi wa piramidi unabaki kutokuelewa kwamba usanifu wa namna ile wa watu wa kale wamewezaje? kwa sababu jiwe moja lililotumika lilichongwa kwa namna ilifaa kuwa na sehemu yoyote unayoona haikuvutii ilitakiwa iwe hivyo sawa na sababu mbali mbali za kiujenzi, walitumia nini kufanya hivyo au vifaa gani kufanikisha, uchongaji wao wa mawe na masanamu ni wa ajabu mno. Ujenzi wa majengo marefu bado uliendelea kusumbua mpaka ugunduzi wa vyuma imara vyepesi vilipoingia lakini bado hatari ni kubwa hasa kama jengo ni refu linakuwa katika hatari za upepo na kutitia ardhini kama usanifu wake hautazingatiwa vizuri. Lakini bado fedha za ujenzi wa sasa hutokana na ufadhili, mikopo mikubwa watu au mataifa huiingia, lakini ujenzi wa falme za zamani ulitegemea raslimali kutoka sehemu alizotawala kwa sababu hakuna adui unayemuwinda atakupa mkopo wa kujiimarisha. Mwenyezi Mungu amewafuta wote hawa na elimu na uzoefu wao na kutuachia sisi athari zao.

Hata siku za sasa watu wanahangaika mno kuhusu gunduzi zinazotokea hasa akili bandia (AI) au maroboti ambayo wanadhani yatakuja kuchukua sehemu za wanadamu na umuhimu wao, historia ni shahidi kuwa watu walipojiona wana nguvu Fulani walipigwa na kurudishwa alifu tena.

Mwenyezi Mungu anasema:

Je, hawatembei katika nchi na kuona jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? **wao walikuwa wenye nguvu zaidi kuliko hawa, na wakiilima ardhi na kuistawisha zaidi kuliko hawa walivyostawisha,** na Mitume wao waliwafikia kwa dalili waziwazi, basi hakuwa Mwenyezi Mungu wa kuwadhulumu, lakini walikuwa wenyewe wakijidhulumu. **(30:10)**

Maneno haya yanaongea nasi kwa sauti kubwa mno, kwani watu waliopita kabla yetu walikuwa na nguvu na walifanya makubwa kwa sababu nyenzo walikuwa nazo na nguvu na maarifa kuliko sisi, lakini kosa walilolifanyia nafsi zao ni kukataa sauti iliyokuwa inawaunganisha na Mwenyezi Mungu, ambaye ndio chanzo cha kila kitu walichokuwa na uwezo nacho, ni sauti ya kunyenyekeza mno na kwa kuona haya majengo roho yenye hofu huanguka chini.

Tuliingia katika Jama Masjid na kukata kiu zetu na kupiga picha nyingi kabla ya kuambiwa tutoke nje kwani muda wa kufunga ulikuwa tayari ushawadia, vijana wengi walituomba tupige picha nao kwani katika India nasi tuligeuka kama wazungu vile wanapokuja kutembelea Afrika. Walitushangaa na walivutika kupiga picha nasi, binafsi yangu nilimpa kila mtu nafasi ya kupiga picha nami, niliacha usambaa na mwinyi wake nyumbani. Kheri, tulipokuwa tunanunua bidhaa nje Mzee mmoja ambaye alikuwa anatuuzia katika maongezi na kujitambulisha nilipomuambia naitwa Shabani alijawa na furaha na kusema unajina sawa imamu wa Jama Masjid ambaye anaitwa Syed Shaban Bukhari, lakini sio kitu cha fahari kwangu, kwani mwenyezi Mungu amenibariki kuwa mtumishi wake chini wa Imamu wa zama na nidhamu ya Ukhalifa.

Roho yangu ilikataa kabsa na haikuwa na shauku ya kusali katika ule msikiti, kuna kitu kizito ndani yangu, hasa sauti iliyokuwa inanisumbua ndani yangu ni kwamba Allah aliwapokonya waislamu lile jengo ambalo ilikuwa ni alama ya utawala wao, nimeumia mno kuona Mwenyezi Mungu alivyowafadhili waislam na wakajisahau, hivyo sikuweza kufurahia kabisa uwepo wangu katika Jama Masjid, hata siku ya pili nilipokuja wakati narudi nyumbani kutoka Qadian tulienda na nilihisi maumivu ya namna zaidi na zaidi kwa sababu watalii walikuwa wanatembea huku na kule na hata wakati wa ibada ulipowadia watu walikuwa wanaendelea na shughuli zao, binafsi nilikataa wazo la kusali katika msikiti ule.

Usanifu majengo wa nchini India unaonekana katika kila kona, nimestaajabu mno kwamba hata fremu za duka ni kubwa mno kuliko kawaida tuliyozoea huku kwetu, na majengo makubwa makubwa mno yanaonekana kila sehemu, kuanzia mahekalu ya kuabudia ukubwa wake na nakshi zake zinaonyesha ukubwa wa usanifu wao. Mwalimu Salehe Yaasin ni mwanahistoria na muandishi wa vitabu aliyefanyanikiwa mno nchini kwa uandishi wake, alipohudhuria katika Jalsa salana ya Qadian nilipata kuongea naye katika hili naye akaeleza kuwa kwa kufika Qadian kulimpa uhalisia wa vitu vingi alivyovisoma kuhusu usanifu majengo wa India,

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE







SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Na.
Sheikh Shaban Othman Shunda



Basi tulipofika Delhi nilianza kumlaumu Sheikh Ayyaz sahib, kwanini ameninunulisha makoti mengi kwa ajili ya safari hii wakati hamna baridi yoyote ya kutisha? Akawa ananiambia kwa mzaha kuwa 'namuomba Mungu awaonyeshe baridi ni nini kabla ya kurudi', Alhamdulilla hapa ninavyoandika hii makala nimejifunika blanketi lenye uzito wa godoro la tatu kwa sita na koti na mzula kichwani na nipo ndani nimejifungia, na huko nje kuna ukungu wa hatari, nimevua glavu mkononi ili niweze kutumia laptop kuandika waila haitakiwi sehemu yoyote ya mwili kuwa wazi, namshukuru Mungu kwa kunionjesha baridi ambayo sikuwahi kuihisi tangu nizaliwe na kwa mara ya kwanza katika mji na nchi ya Masihi aliyeahidiwa[as]. Tulipokuwa Delhi siku ya kwanza usingizi nilioupata ulikuwa mzito mno na ndoto nilizoona zilikuwa za wazi na safi mno, uzito wake na uwazi wake ilikuwa ni tofauti sana na kawaida na uzoefu wangu. Ilibidi niwaeleze wenzangu pale chumbani kwa kauli moja kuwa, 'ardhi na mazingira haya yana uwezo mkubwa wa mtu kupata wahyi kutoka kwa Mungu', papo hapo wote tukaanza kuchangia na kuunga mkono kuwa ni kweli sehemu nyingi ambazo manabii wa Mwenyezi Mungu walipodhihiri kuna sifa hii ya hali ya hewa, hali ya hivi kwamba wakati wa joto huwa joto kali mno lakini wakati wa baridi pia unakuwa wa baridi kali mno, ukiangalia katika maisha ya mitume na mazingira yao jambo hili linakuwa wazi zaidi. Ukiachilia mbali hilo, Delhi pia ni nyumbani kwa mawalii wengi wa Mungu kama vile Hadhrat Bukhtiar kaki r.h, Hadhrat Nidhamuddin Auliyaa r.h, Hadhrat Shah Waliyullah r.h, n.k ambao walipata heshima ya kuongea na kuongozwa na Mwenyezi Mungu ambapo pia kuna alama kubwa za maendeleo ya uislamu katika zama zake za kati.

Siku ya pili mjini Delhi tuliamua kutoka na kwenda kuzunguka na pia tulitaka kubadili hela na kununua vifaa kadhaa, tuliongozana na sheikh mmoja na mwalimu mmoja wa Jamaat ambao walikuwa katika ziara ya kikazi kuzungukia Jamaat za India, basi wakawa wenyeji wetu katika mji wa Delhi, moja kwa moja tukaenda kwenye **Qutb minar** ambapo ni sehemu ya kivutio cha utalii lakini hatukutaka kuingia kwa sababu walikuwa wanatoza kiasi kikubwa cha fedha kwa wageni kulinganisha na wenyeji, tukakubaliana kwenda kubadili fedha kwanza kisha tuelekee sokoni.

Tukapanda treni ya umeme ya chini ya ardhi ambayo mara inapita chini ya ardhi sehemu nyingine inapita juu zaidi na hivyo hivyo vituo vyake kuna vilivyo juu na vingine chini ya ardhi, vingine vipo chini ya ardhi gorofa mpaka mbili lakini vingine viko juu inabidi

UK. 10





Je, Wajua?

Gravity ni hali inayofanya kitu kimoja kivute kitu au vitu vingine kukielekea. Kila kitu kina gravity, Baadhi vina gravity kubwa kuliko vingine. Vyenye gravity kubwa huvuta vyenye ndogo. Mwanadamu na kila kilichopo ardhini huvutwa kuelekea chini ya dunia kwa sababu gravity imeshinda katika vita ya mvutano. Ndio maana huwezi kurusha jiwe likaelekea juu tu bila kurudi chini. Ukiruka pia lazima utarudi chini. Vivyo hivyo, Jua lina gravity kubwa kuliko dunia, na jua huvuta dunia kuielekea. Kinachofanya dunia isivutwe na kumezwa na jua ni kwa sababu inalizunguka jua kwenye mhimili fulani. Vivyo hivyo, dunia ina gravity kubwa kuliko mwezi na ingeweza kuuvuta mwezi kama mwezi usingekuwa unaizunguka dunia. Satellite pia hazianguki duniani kwa sababu zinaizunguka dunia kwenye mhimili. Gravity inategemea ukubwa na uzito wa kitu. Mfano, uzito na ukubwa wa dunia hufanya gravity ya dunia kuwa ilivyo na jua vivyo hivyo.

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 10,000/=.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com